

KITABU
CHA NABII DANIELI.

SO
LI
DEO
GL
OR
IA

ZANZIBAR,
1882.

DANIELI.

MWAKA wa tatu wa kumiliki kwake Yehoyakim, mfalme wa Yuda, alikuja Nebukadnezar, mfalme wa Babel, kwa Yerusalemi, akauzunguka.

2 Yahuwa akatoa Yehoyakim, mfalme wa Yuda, mkononi mwake, na katika vyombo vya nyumba ya Muungu, alivyovichukua inchi ya Shinar nyumbani kwa muungu wake, akavileta vyombo kwenyi hazina za muungu wake.

3 Mfalme akamwambia Aspenaz mkuu wa matoashi wake, awalete katika waana wa Israeli, na uzao wa kifalme, na walio wa

4 kwanza, vijana, wasio na mawaa, na wazuri, wenyi moyo wa hekima, na werevu kwa akili, na wenyi kujua elimu, watakaoweza kusimama jumbani mwa mfalme, wapate kuwafundisha maandiko na lugha ya Wa-

5 kasidi. Mfalme akawaagizia posho ya killa siku ya chakula cha mfalme, na ya mvinyo

DANIELI, I.

wa kinywa chake, akawalisha miaka mitatu, hatima yake wasimame mbele ya mfalme.

6 Bassi katika hawa walikuwako wa waana wa Yuda, Danieli, na Ananiya, na Misael, na

7 Azariya. Nao akawatia majina mkuu wa matoashi, akampa Danieli Belteshazar, na Ananiya Shadrach, na Misael Meshach, na A-

8 zariya Abed-nego. Bassi Danieli akakusudi moyoni mwake, asijitie uchafu na sehemu ya chakula cha mfalme, wala na mvinyo alionywa: kwa sababu hii akamtaka mkuu wa

9 matoashi asijitie uchafu. Muungu akawa amemletea Danieli upendeleo na shauko

10 kwa mkuu wa matoashi. Na mkuu wa matoashi akamwambia Danieli, Namwogopa bwana wangu, mfalme, aliyewaagizia chakula chenu, na kinywa chenu. Mbona azione nyuso zenu za huzuni kuliko waana wa zamu yenu? Ndipo mtaniingiza hatarini

11 kitwa changu kwa mfalme. Danieli akamwambia wakili, aliyemweka mkuu wa matoashi juu yao Danieli, na Ananiya, na Mi-

12 sael, na Azariya, Bassi uwajaribu, nakusihi, watumwa wako siku kumi, wakatupe cha

DANIELI, I.

- 13 mtama tukile, na maji tuyanywe. Tuka-
tazamiwe nyuso zetu mbele yako, na nyuso
za waana walao posho ya chakula cha mfal-
me, nawe, utakavyoona, uwatendee watu-
14 mwa wako. Akawasikia kwa jambo hili,
15 akawajaribu siku kumi. Mwisho wa siku
kumi wakaonekana nyuso zao wazuri na
wamenenepa kuliko waana wote waliokula
16 posho ya chakula cha mfalme. Wakili aka-
watwalia posho yao ya chakula, na mvinyo
17 wa kunywa kwao, akawapa mtama. Bassi
wale watoto wanne Muungu akawapa elimu
na akili katika maandiko yote na hekima,
akamjulisha Danieli njozi zote, na ndoto.
18 Hatta siku zikiisha, alizozinena mfalme za
kuwaingiza, akawaleta mkuu wa matoashi
19 mbele yake Nebukadnezar. Mfalme aka-
zumgumza nao, wala miongoni mwao wote
hawakuonekana walio sawa na Danieli, na
Ananiya, na Misael, na Azariya. Bassi wa-
20 kasimama mbele ya mfalme. Na kwa ma-
mbo yote ya hekima na kutambua, aliyo-
wauliza mfalme, akawaona wamepita marra
kumi wachawi na wanajimu wote wa ufalme

DANIELI, II.

21 wake pia. Danieli akadumu hatta kwa mwaka wa kwanza wa mfalme Kuro.

II. Mwaka wa pili wa kumiliki kwake Nebukadnezar, Nebukaduezar akaota ndoto, roho yake ikafathaika nazo, usingizi wake
2 ukamwondokea. Bassi mfalme akaamuru wawaite wachawi, na wanajimu, na waganga, na Wakasidi, wamwonyeshe mfalme ndoto zake. Wakaja wakasimama mbele ya
3 mfalme. Mfalme akawaambia, Nimeota ndoto, roho yangu ikafathaika nijue ndoto.
4 Bassi Wakasidi wakamwambia mfalme kwa Kishami, Ee mfalme, uishi milele, uwaambie watumwa wako ndoto, nasi tutaonyesha
5 tafsiri. Mfalme akajibu akawaambia Wakasidi, Neno limetoka kwangu, msiponijulisha ndoto na tafsiri yake, mtakatwa vipande vipande, na nyumba zenu zitafanyika
6 jaa. Lakini kama mtanionyesha ndoto, na tafsiri yake, mtapewa nami zawadi na ijara na heshima kuu : bassi nionyeshe ndoto na tafsiri yake. Wakajibu tena waka-
7 sema, Mfalme atwambie watumwa wake ndoto, nasi tutaonyesha tafsiri yake.

DANIELI, II.

- 8 Mfalme akajibu akasema, nimejua kwa kweli kama mnakomboa wakati, kwa sababu mmeona jambo limetoka kwangu.
- 9 Lakini msiponijulisha ndoto, amri moja kwenu, kwani mmejiwekea maneno ya uwongo na maovu ya kusemea mbele yangu, hatta wakati ubadilike. Bassi mniambie ndoto, nami nitajua, kama mnaweza
- 10 kunionyesha tafsiri yake. Wakasidi wakajibu mbele ya mfalme, wakasema, Hapana mtu duniani awezaye kuonyesha neno la mfalme: bassi wala mfalme, wala mkubwa, wala liwali, hajauliza kama haya wala kwa mchawi, wala kwa mnajimu, wala kwa
- 11 Mkasidi. Jambo hilo zito mfalme atakalo, wala hapana mwingine awezaye kulionyesha mbele ya mfalme, illa miungu, wasio-
- 12 kaa katika mwili. Bassi mfalme akaona hasira na ghathabu nyingi, akaamuru waharibu wenyi hekima wote wa Babel.
- 13 Amri ikatoka wenyi hekima wauawe, wakamtafuta Danieli na wenzake wauawe.
- 14 Ndipo Danieli akamjibu kwa busara na hekima Ariok, mkuu wa asikari za mfalme,

DANIELI, II.

- aliyetoka awaue wenyi hekima wa Babel,
15 akajibu akamwambia Ariok, akida wa
mfalme, Mbona amri imetoka na haraka
kwa mfalme? Ariok akamjulisha Danieli
16 jambo. Bassi Danieli akaingia akamtaka
mfalme amwachilie nafasi, naye atamjuli-
17 sha mfalme tafsiri. Danieli akaenda nyu-
mbani kwake akawajulisha jambo Ananiya,
18 na Misael, na Azariya, wenzake: wamtakie
huruma Muungu wa mbinguni kwa siri hii;
wasiwaharibu Danieli na wenzake pamoja
na wangine wenyi hekima wa Babel.
- 19 Ndipo akafunuliwa siri Danieli katika
matokeo ya usiku. Danieli akambariki
Muungu wa mbinguni. Danieli akajibu
akasema, Libarikiwe jina la Muungu milele
na milele: kwani hekima na nguvu ni zake.
21 Ndiye abadiliye wakati na muhulla, huondoa
wafalme, huwainua, huwapa hekima wenyi
22 hekima, na akili wenyi kutambua. Hufu-
nua mambo ya chini na ya siri, yaliyomo
gizani huyajua, na nuru inakaa naye.
23 Wewe, Ee Muungu wa baba zangu, naku-
shukuru, nakusifu, kwani umenipa hekima

DANIELI, II.

na nguvu, umenijulisha tuliyokutakia, kwa-
24 ni umetujulisha jambo la mfalme. Bassi
Danieli akaenda kwa Ariok, mfalme aliye-
mwagiza awaharibu wenyi hekima wa Ba-
bel, akaenda akamwambia hivi, Usiwa-
haribu wenyi hekima wa Babel, nichukue
mbele ya mfalme, nami nitamwonyesha
25 mfalme tafsiri yake. Ndipo Ariok aka-
mchukua Danieli mbele ya mfalme kwa
haraka akamwambia hivi, nimeona mtu
wa waana wa mateka wa Yuda, atakaye-
26 mjulisha mfalme tafsiri yake. Mfalme
akajibu, akamwambia Danieli, jina lake
Belteshazar, Waweza kunijulisha ndoto ni-
27 liyoona na tafsiri yake? Danieli akajibu
mbele yake mfalme, akasema, siri aliyoiu-
liza mfalme, hawawezi wenyi hekima, wa-
najimu, wachawi, wabashiri, kumwonye-
28 sha mfalme; illakini yuko mbinguni Muu-
ngu afunuaye siri, naye amemjulisha mfal-
me Nebukadnezar yatakayokuwa siku za
mwisho. Ndoto yako, na matokeo ya kitwa
29 chako kitandani mwako, ndizo hizi; Wewe,
Ee Mfalme, mawazo yako yalikuja kita-

DANIELI, II.

ndani mwako, vitakavyokuwa halafu, naye afunuliaye siri akujulisha yatakavyokuwa.

30 Nami, si kwa hekima kwa kuwa nayo kuliko wahayi wengine nimefunuliwa siri hii, illa wapate kumjulisha mfalme tafsiri yake,

31 ukayajue mawazo ya moyo wako. Wewe, mfalme, walikiona, na tazama mfano mmoja mkubwa. Mfano huu mkubwa, kun'gaa kwake bora, ukasimama mbele yako, na

32 sura yake yenyi kuogofya. Mfano huu, kitwa chake cha thahabu safi, kifua chake na mikono yake ya fetha, tumbo lake na

33 mapaja yake ya shaba. Miguu yake ya chuma kwa juu, na kwa chini nusu ya

34 chuma na nusu ya udongo. Ukaona, hatta lilipokatika jiwe, lisimo mikononi, likaupiga mfano miguu yake ya chuma na udongo,

35 likaivunjavunja. Ndipo chuma, udongo, shaba, fetha, thahabu, zikavunjikavunjika, zikawa kama makapi ya sakafu za mavuno, upepo ukazichukua, pasionekane mahali pao; nalo jiwe lililoupiga mfano, likawa

36 mlima mkubwa, ukaijaza inchi yote. Hii ndiyo ndoto, naswi tutainena tafsiri yake

DANIELI, II.

37 mbele ya mfalme. Wewe, Ee mfalme, mfalme wa wafalme: kwani Muungu wa mbinguni amekupa ufalme na uwezo na
38 nguvu na utukufu. Na wakaapo pote waa-na Adamu, nyama za koondeni, na ndege za mbingu, amezitoa mkononi mwako, amekufanya bwana juu yao yote. Wewe kitwa
39 hiki cha thahabu. Na nyuma yako utao-ndoka ufalme mwingine usiolingana nawe. Na ufalme mwingine wa tatu wa shaba
40 utakaotawala juu ya inchi yote. Na ufalme wa 'nne utakuwa wa nguvu kama chuma, na ginsi chuma kivunjavyo, kipondavyo vyote, kama chuma kivunjavyo, ndivyo utakavyoponda na kuvunja hizi zo-
41 te. Na kama ulivyoiona miguu na vidole, nussu udongo wa mfinyangi, na nussu chuma, ufalme utagawanyika, lakini zitakuwamo za nguvu za chuma, kama ulivyoona chuma kimechanganyika na udongo wa
42 tope. Na vidole vya miguu nussu chuma, nussu udongo: ufalme nussu mwenyi nguvu,
43 nussu uvunjikao. Na kama ulivyoona chuma kimechanganyika na udongo, watajicha-

DANIELI, II.

nganya na wazao wa watu, wasishikane huyu na huyu, hatta kama chuma hakicha-
44 nganyikani na udongo. Na siku zao wa-
falme hawa Muungu wa mbinguni atasi-
mamisha ufalme usioharibika milele, na
ufalme wake hawataachiliwa wangine, uta-
zipigapiga na kuziharibu falme hizi zote,
45 nao utakaa milele. Na ulivyoona jiwe li-
mekatika mlimani lisimo mikononi, likazi-
vunjavunja chuma, na shaba, na udongo,
na fetha, na thahabu, Muungu aliye mkuu
amemjulisha mfalme yatakayokuwa baa-
daye: nayo kweli ndoto, na tafsiri yake
amini.

46 Ndipo mfalme Nebukadnezar akaanguka
usoni mwake, akamsujudia Danieli, akaa-
47 muru wamtolee sadaka na uvumba. Mfalme
akajibu akamwambia Danieli, Hakika Mu-
ungu wenu Muungu wa miungu na bwana
wa wafalme, afumbuaye siri, ukiwa umewe-
48 za kuifunua siri hii. Bassi mfalme akan-
tu-
kuza Danieli, akampa zawadi kuu nyingi,
akamfanya mkubwa juu ya inchi yote ya
Babel. Na wa kwanza wa maliwali juu

DANIELI, III.

49 yao wote wenyi hekima wa Babel. Danieli akamtaka mfalme, akawaweka Shadrak, na Meshak, na Abednego, juu ya mambo yote ya inchi ya Babel, lakini Danieli mlangoni mwa mfalme.

III. Nebukadnezar mfalme akafanya mfano wa thahabu, urefu wake mikono settini, upana wake mikono sita, akauweka kwa inchi sawa ya Dura katika inchi ya Babel.

2 Nebukadnezar mfalme akapeleka awakusanye maliwali, na majemadari, na maakida, na makathi, na watunza hazina, na madiwani, na waamuzi, na wakuu wote wa inchi, waje kwa kuwekea wakf mfano Nebuka-

3 dnezar mfalme aliouweka. Bassi maliwali, na majemadari, na maakida, na makathi, na watunza hazina, na madiwani, na waamuzi, na wakuu wote wa inchi wakakusanyika kwa kuwekea wakf mfano Nebukadnezar mfalme aliouweka, wakasimama mbele ya mfano Nebukadnezar aliouweka.

4 Bassi mjumbe akalia na nguvu, Ninyi waamuru, enyi watu, na mataifa, na ndimi,

5 wakati mtakaposikia sauti ya baragumu, na

DANIELI, III.

filimbi, na kinubi, na zeze, na kinanda, na zomari, na namna zote za ngoma, mwanguke mwnsujudie mfano wa thahabu, Nebukadnezar mfalme aliouweka. Na yee yote asiyeanguka asiyesujudu, saa ileile atatu-
6 pwa kati ya tanuu la moto uwakao. Bassi wakati ule watu wote waliposikia sauti ya baragumu, na filimbi, na kinubi, na zeze, na kinanda, na namna zote za ngoma, watu wote, na mataifa, na ndimi, wakaanguka, wakausujudia mfano wa thahabu Nebukad-
8 nezar mfalme aliouweka. Bassi ndipo wakakaribia watu Wakasidi, wakawashtaki
9 Wayahudi. Wakanena, wakamwambia mfalme Nebukadnezar, Ee mfalme, uishi milele. Wewe, mfalme, umetoa amri, killa mtu atakayesikia sauti ya baragumu, na filimbi, na kinubi, na zeze, na kinanda, na zomari, na namna zote za ngoma, aanguke,
11 ausujudie mfano wa thahabu; naye yote asiyeanguka, asiyesujudu, atupwe kati ya
12 tanuu la moto uwakao. Kuna watu, Wayahudi, uliowaweka juu ya mambo ya inchi ya Babel, Shadrak, na Meshak, na Abed-

DANIELI, III.

nego; watu hawa, Ee mfalme, hawakukua-
ngalia wewe: hawatumikii miungu yako,
wala hawausujudii mfano wa thahabu ulio-
uweka.

- 13 Bassi Nebukadnezar mwenyi hasira na
ghathabu akaamuru wawaleta Shadrak, na
Meshak, na Abednego. Wakawaleta watu
14 hawa mbele ya mfalme. Akanena Nebu-
kadnezar, akawaambia, Kwa maksudi, enyi
Shadrak, na Meshak, na Abednego, ham-
tumikii miungu yangu, wala hamwusujudii
15 mfano wa thahabu niliouweka? Bassi ka-
ma mtakuwa tayari wakati mtakaposikia
sauti ya baragumu, na filimbi, na kinubi,
na zeze, na kiranda, na zomari, na namna
zote za ngoma kuanguka na kusujudia mfa-
no niliufanya, lakini msiposujudu mtatu-
pwa saa ileile kati ya tanuu la moto uwakao;
na nani Muungu yule atakayewaokoa kati-
16 ka mikononi mwangu? Wakajibu Shadrak,
na Meshak, na Abednego, wakamwambia
mfalme, Ee Nebukadnezar, hatuna haja sisi
17 kukujibu kwa jambo hilo. Ijapokuwa,
Muungu wetu, tumtumikiaye, anaweza ku-

DANIELI, III.

tuokoa katika tanuu la moto uwakao, naye atatuokoa katika mikononi mwako, Ee mfalme, 18 lme. Ama siwyo, ijulike kwako, Ee mfalme, hatutaabudu miungu yako, wala hatutausujudia mfano wa thahabu uliouweka.

19 Ndipo Nebukadnezar akajaa ghashabu, na sura ya uso wake imebadilika juu yao Shadrak, na Meshak, na Abednego, akane-

20 ba kupita desturi yake ya kutiwa moto.

Akaamuru mashujaa wa nguvu wa jeshi lake wawafunge Shadrak, na Meshak, na Abednego, kutupwa katika tanuu la moto u-

21 wakao. Bassi watu hawa wakafungwa na kanzu zao na joho na vitambi, na nguo zao, wakatupwa kati ya tanuu la moto uwakao.

22 Na tena sababu neno la mfalme likawa na nguvu, tanuu ikawaka sana, ndimi za moto zikawaua wale watu waliowachukua Sha-

23 drak, na Meshak, na Abednego. Hawa watatu Shadrak, na Meshak, na Abednego, wakaanguka wamefungwa kati ya tanuu la

24 moto uwakao. Ndipo Nebukadnezar akashangaa, akaondoka kwa haraka, akinena,

DANIELI, III.

- akiwaambia watu wake wa baraza, Si watu watatu tuliowatupa wamefungwa kati ya moto? Wakajibu wakamwambia mfalme,
- 25 Kweli, Ee mfalme. Akajibu, akasema, Tazama, nawaona wanne wamefunguliwa, wاناتembea kati ya moto, wala haimo matharra mwao; na sura yake wa 'nne imefanana na mwana wa Muungu.
- 26 Ndipo Nebukadnezar akakaribia mlango ni mwa tanuu la moto uwakao akanena, akasema, Shadrak, na Meshak, na Abednego, enyi watumwa wake Muungu aliye juu, tokeni, mkaje. Bassi Shadrak, na Meshak, na Abednego, wakatoka katika kati ya moto.
- 27 Na maliwali, na majemadari, na maa-kida, na madiwani wa mfalme wakikusanyika pamoja, wakawaona watu hawa, juu ya miili yao moto haukuwa na nguvu, wala unyele wa kitwa chao haukuunguliwa, wala kanzu zao hazikubadilika, wala manuka ya
- 28 moto hayakuzipata. Akanena Nebukadnezar, akasema, Abarikiwe Muungu wa Shadrak, na Meshak, na Abednego, aliye peleka malaika wake, akawaokoa watumwa

DANIELI, IV.

wake waliomtumainia, waliobadili neno la mfalme, wakatoa miili yao, wasitumikie wala kusujudia muungu wo wote, illa Muungu wao wenyewe. Bassi amri imefanyika kwangu, killa kabila, na taifa, na ulini, wasemao kosa juu ya Muungu wa Shadrak, na Meshak, na Abednego, watakatwakatwa, na nyumba zao zitafanywa jaa: kwani hapana Muungu mwingine awezaye kuokoa kwa ginsi hiyo. Ndipo mfalme akawafanikisha Shadrak, na Meshak, na Abednego, katika inchi ya Babel.

IV. Nebukadnezar mfalme kwa watu wote, na mataifa, na ndimi, wakao katika dunia yote; amani kwenu izidi. Ishara na matajabu Muungu aliye juu alizofanya nami, ilipendeza mbele yangu nizingaze. Ishara zake ginsi zilivyo kuu! matajabu yake ginsi ya nguvu! ufalme wake ufalme wa milele, na mamlaka yake kizazi kwa kizazi. Mimi Nebukadnezar, nilikistarehe nyumbani kwangu, nikasitawi jumbani mwangu. Nikaona ndoto, iliyoniogofisha, mawazo ya kitandani mwangu, na njozi za

DANIELI, IV.

- 6 kitwa changu zikanifathaisha. Bassi nika-
fanya amri kuwaleta wenyi hekima woto
wa Babel mbele yangu, wanijulishe tafsiri
7 yake ndoto. Wakaja wachawi, na wana-
jimu, na Wakasidi, na wabashiri, nikaitoa
ndoto mbele yao, wasinijulishe tafsiri yake.
8 Hatima yake akaingia Danieli mbele yangu,
mwenyi jina la Beltesazar kwa jina la
muungu wangu, kwake roho ya miungu
9 watakatifu, nikatoa mbele yake ndoto. Eo
Beltesazar, mkuu wa wachawi, kwa saba-
bu najua, kwako roho ya miungu watakatifu,
wala hapana siri ikutaabishayo, uniambie
njozi za ndoto niliyoiona na tafsiri yake.
10 Hivi njozi za kitwa changu kitandani
mwangu : nilikiona, na tazama, mti kati ya
11 inchi, na urefu wake mkubwa. Mti ukakua
ukasitawi, urefu wake ukafika mbingu-
ni, ukaonekana hatta mwisho wa dunia yote :
12 Majani yake mazuri, na matunda yake mengi,
na ndani yake chakula kwa wote :
nyama za koondeni zikawa na kivuli chini
yake, ndege za mbingu zikakaa katika matawi
13 tawi yake, miili yote ikalishwa nao. Nika-

DANIELI, IV.

ona katika njozi za kitwa changu kitandani
mwangu, na tazama, mkesha naye mtakati-
14 fu, akashuka mbinguni; akalia na nguvu,
akasema hivi, Uukate mti, ukafeke matawi
yake, ukatikisie mbali majani yake ukata-
wanye matunda yake : ziondoke nyama kati-
ka chini yake, na ndege katika matawi yake.
15 Illakini uliache shina la mizizi yake katika
inchi, hatta kwa kufunga na chuma na sha-
ba, katika majani meroro ya koondeni, li-
katiwe maji na umande wa mbinguni, na
sehemu yake kwa nyama katika majani ya
16 inchi : Moyo wake ubadilike katika moyo
wa mwana Adamu, na moyo wa nyama a-
17 pewe, nyakati saba zikampitie. Jambo hili
kwa amri ya wakesha, na haja kwa neno
la watakatifu : wapate wahayi kujua kama
aliye juu ndiye atawalaye ufalme wa waana
Adamu, humpa yee yote ampendaye, huweka
18 juu yake walio wanyonge. Ndoto hii mimi
mfalme Nebukadnezar nimeiona. Bassi sa-
sa, Ee Belteshazar, ueneze tafsiri yake,
kwani wenyi hekima wote wa ufalme wa-
ngu hawawezi kunijulisha tafsiri, wewe

DANIELI, IV.

ndiwe uwezaye; kwani kwako roho ya
19 miungu watakatifu. Bassi Danieli, jina lake Belteshazar, akashangaa dakika moja, mawazo yake yakamtaabisha. Mfalme akana, akasema, Belteshazar, ndoto isiku-taabishe, wala tafsiri yake. Belteshazar, akajibu akasema, Bwana wangu, ndoto kwao wakuchukia, na tafsiri yake kwa adui
20 zako. Mti uliouona unakua, ukasitawi, urefu wake ukafika mbinguni, ukaoneka-
21 na kwa dunia yote; majani yake mazuri, na matunda yake mengi, na ndani yake chakula kwa wote; chini yake nyama za inchi zikakaa, juu ya matawi yake ndego
22 za mbingu zikawa na makao yao: Ndiwe wewe, Ee Mfalme, uliyekua ukasitawi: kwani ukuu wako umesitawi, wafika mbinguni, na mamlaka yako hatta mwisho wa
23 dunia. Na ikiwa mfalme akaona mkeshana naye mtakatifu akishuka mbinguni, na kusema, Ukate mti, ukauharibu, illa liacho shina la mizizi yake katika inchi, hatta kwa kufungwa na chuma na shaba, katika majani meroro ya koondeni; likatiwe maji na

DANIELI, IV.

umande wa mbinguni, na sehemu yake
na nyama za mwitu, hatta nyakati saba
24 zimpitie; Hii tafsiri, Ee mfalme, na hii
amri yake aliye juu, iliyomjia bwana wa-
25 ngu mfalme: Ya kwamba watakufukuza
katika watu, na makao yako yatakuwa na
nyama za mwitu, na watakulisha majani
kama ng'ombe, na watakutia maji na uma-
nde wa mbinguni, na nyakati saba zitakupi-
tia, hatta utakapojua, kama aliye juu ndiye
atawalaye ufalme wa waana Adamu, humpa
26 yee yote ampendaye. Na ikiwa wameamuru
kuacha shina la mizizi ya mti; ufalme wa-
ko utakuwa imara kwako, baada yake uta-
kapokwisha kujua kama mbingu ndizo zi-
27 tawalazo. Kwa ajili hii, Ee Mfalme, shauri
langu likubalike kwako, ukajivunjie thambi
kwa haki, na maovu yako kwa kuwarehe-
mia masikini; iwe labda kuzidisha raha
yako.
28 Haya yote yakamjia mfalme Nebukadne-
29 zar. Miezi thenashara ikiisha akatembea
30 juu ya jumba la ufalme wa Babel. Mfalme
akanena akasema, Si huu Babel mkuu ni-

DANIELI, IV.

lioujenga mimi kuwa nyumba ya ufalme
kwa uwezo wa nguvu zangu, na kuwa utu-
31 kufu wa enzi yangu. Hatta neno likiwamo
kinwani mwa mfalme, ikashuka sauti katika
mbinguni. Ee mfalme Nebukadnezar, kwa-
32 ko lauenwa; Ufalme umekuondokea. Nao
watakufukuza katika watu, na makao yako
na nyama za koondeni: watakulisha majani
kama ng'ombe, na nyakati saba zitakupitia,
hatta utakapojua ya kwamba aliye juu ndiye
atawalaye ufalme wa waana Adamu, humpa
33 yee yote ampendaye. Dakika ileile jambo
likatimizwa juu yake Nebukadnezar: aka-
fukuzwa katika watu, akala majani kama
ng'ombe, mwili wake ukatiwa maji na uma-
nde wa mbinguni, hatta nyele zake zikakua
kama tai, na kucha zake kama za ndege.
34 Mwisho wa siku mimi Nebukadnezar nika-
yainua macho yangu mbinguni, akili za-
ngu zikanirudia, nikambariki aliye juu,
nikamsifu, nikamheshimia, aishiye milele,
mamlaka yake mamlaka ya milele, na ufalme
35 wake kizazi na kizazi: na wakao wote
duniani kuhesabiwa kama si kitu: naye

DANIELI, V.

atendaye kwa mapenzi yake katika jeshi la mbinguni, na wakaao duniani: wala hapana awezaye kumzuia mkono: ao kumwa-
36 mbia, Wafanyaje? Wakati uleule akili zangu zikanirudia; na kwa utukufu wa ufalme wangu heshima yangu na enzi yangu zikanirudia; na madiwani wangu na wakuu wangu wakaniamkia; nikawekwa imara katika ufalme wangu, nikazidishiwa
37 enzi bora. Nami sasa Nebukadnezar namsi-fu, namtukuza, namheshimia Mfalme wa mbingu, kazi zake zote kweli, na njia zake hukumu: nao waendao na kiburi aweza kuwashusha.

V. Belshazar mfalme akawafanyia karamu kubwa wakuu wake elfu, akanywa mvinyo
2 mbele yao elfu. Belshazar alipokionja mvinyo akaamuru wavilete vyombo vya thahabu, na vya fetha, baba yake Nebukadnezar alivyovitwaa katika hekalu la Yerusalemi; wapate mfalme, na wakuu wake, na wakewe, na masuria yake, kuvinywea.

3 Bassi wakavileta vyombo vya thahabu, vilivyotwaliwa katika hekalu la nyumba ya

DANIELI, V.

Muungu katika Yerusaleimi; na mfalme na
4 wakuu wake, na wakewe, na masuria yake,
wakavinywea. Wakanywa mvinyo, wakaisifu miungu ya thahabu, na ya fetha, na ya shaba, na ya chuma, na ya mti, na ya mawe.
5 Saa ileile vikatoka vidole vya mkono wa mtu, vikaandika karibu na taa katika chokaa ya ukutani mwa jumba la mfalme: mfalme akaiona ncha ya mkono ulioandika.
6 Bassi uso wake mfalme umebadilika, mawazo yake yakamfathaisha, hatta mafungo ya viuno vyake yakalegea, na magote yake
7 yakagonganagongana. Mfalme akalia na nguvu kuwaleta wanajimu, na Wakasidi, na wabashiri. Mfalme akanena, akawaaambia wenyi hekima wa Babel, Awaye yote atakayesoma andiko hili, na kanionyesha tafsiri yake, atavikwa porfuro, na mkufu wa thahabu shingoni mwake, naye atakuwa
8 mtawala wa tatu katika ufalme. Bassi wenyi hekima wote wa mfalme wakaja wasiweze kulisoma andiko, wala kumjulisha
9 mfalme tafsiri yake. Ndipo mfalme Belshazar akataabika sana, uso wake ukabadilika

DANIELI, V.

kwake, wakuu wake wakafathaika.

- 10 Akaja na malkia, kwa ajili ya maneno ya mfalme na wakuu wake, chumbani kwa kulia: malkia akanena akasema, Ee mfalme, uishi milele, mawazo yako yasikufathaishe,
- 11 wala uso wako usibadilike. Yuko mtu katika ufalme wako, kwake roho ya miungu watakatifu; na katika siku za baba yako wewe nuru na kutambua na hekima, kama hekima ya miungu, zimeonwa kwake; aliye-mweka mfalme Nebukadnezar baba yako, Ee mfalme, baba yako, mkuu wa wachawi,
- 12 wanajimu, Wakasidi, wabashiri; ikiwa roho bora, na elimu, na maarifa ya mtafsiri ndoto, na ya kuonyesha mawosia magumu, na ya mfundua mafundo, zikaonwa kwake Danieli huyu, mfalme aliyemtaja Belteshazar: bassi Danieli aitwe, naye ataionyesha
- 13 tafsiri. Ndipo Danieli akaletwa mbele ya mfalme. Mfalme akanena akanwambia Danieli, Wewe Danieli yule, wa waana wa mateka wa Yuda, mfalme baba yangu alio-
- 14 waleta katika Uyahudi? Hatta nimesikia habari zako, kama roho ya miungu nawe,

DANIELI, V.

na nuru na kutambua na hekima bora ime-
15 onwa kwako. Na sasa wenyi hekima, wa-
najimu, wameletwa mbele yangu, wapate
kusoma andiko hili, na kunijulisha tafsiri
yake: wasiweze kunionyesha tafsiri yake
16 jambo: nami nimesikia habari zako, kama
waweza kutafsiri na kufundua mafundo,
bassi sasa ukiweza kulisoma andiko, na
kunijulisha tafsiri yake, utavikwa porfuro,
na mkufu wa thahabu shingoni mwako, na-
we utakuwa mtawala wa tatu katika ufa-
lme.

17 Danieli akajibu akanena mbele ya mfa-
lme, Zawadi zako ziwe kwako, ukampe mwi-
ngine ijara yako, nami nitamsomea mfalme
18 andiko, nitamjulisha tafsiri. Ewe mfalme,
Muungu aliye juu akampa Nebukadnezar
baba yako ufalme, na enzi, na utukufu, na
19 heshima; na kwa enzi aliyompa, watu wote,
na mataifa, na ndimi, wakatetemeka waka-
ogopa mbele yake: apendaye kumua, hu-
mua, apendaye kumwacha, humwacha hayi,
apendaye kumwinua humwinua, apendaye
20 kumshusha, humshusha. Lakini moyo wa-

DANIELI, V.

ke ulipoinuliwa, na roho yake ikasitawi kuitenda na kiburi, akashushwa katika kiti chake cha kifaume, wakamtwalia utukufu wake;

21 ke; naye akafuknzwa katika waana Adamu; akausawazisha moyo wake na nyama, na makao yake kwa punda za mwitu: wakanlisha majani kama ng'ombe, mwili wake ukatiwa maji na umande wa mbinguni; hatta alipojua kama Muungu aliye juu ndiye atawalaye katika ufalme wa waana Adamu,

22 huweka juu yake ampendaye yote. Nawe mwanawe, Ee Belshazar, hukujithili moyo, hatta ukiwa hali ya kuyajua haya yote;

23 ukajiinua juu yake Bwana wa mbingu: nao wamevileta vyombo vya nyumba yake mbele yako, nawe, na wakuu wako, wakewo, na masuria yako, mmevinywea mvinyo: nawe umeisifu miungu ya fetha, na thahabu, ya shaba, na chuma, na mti, na mawe, isiyoona wala kusikia, wala kujua: naye Muungu, mkononi mwake pumzi yako, na za-

24 ke njia zako zote, hukumtukuza: ndipo ncha ya mkono huu imepelekwa naye; andiko hili likaandikwa.

DANIELI, VI.

25 Nalo andiko lililoandikwa, MENE, ME-
26 NE, TEKEL, UPHARSIN. Hii tafsiri ya-
ke; MENE; Muungu amehesabu ufalme
27 wako, ameumaliza. TEKEL; umepimwa
28 katika mizani, ukaonekana umepunguka.
PERES; ufalme wako umetengwa, ukato-
29 lewa kwa Wamedi na Waajjemi. Bassi Bel-
shazar akaamuru, wakamvika Danieli por-
furo, na mkufu wa thahabu shingoni mwa-
ke, wakamtangazia, awe mtawala wa tatu
katika ufalme.

30 Usiku ule Belshazar, mfalme wa Waka-
31 ldayo akauawa. Na Dario Mmedi akau-
pokea ufalme, mwenyi miaka kama settini
na mbili.

VI. Ikampendeza Dario, aweke juu ya ufalme
maliwali mia na asharini wawe juu ya ufa-
2 lme wote; na juu yao wakubwa watatu,
mmoja wao Danieli: maliwali wapate kutoa
hesabu kwao, mfalme asipate hasara.

3 Bassi Danieli huyu akawatangulia wakuu
na maliwali, kwani roho bora kwake, naye
mfalme akathani kumweka juu ya ufalme
4 wote. Ndipo wakuu na maliwali wakata-

DANIELI, VI.

futa neno juu yake Danieli kwa mambo ya ufalme ; wasione neno wala kosa ; akiwa amini, wala halikuonekana kosa wala neno
5 baya naye. Bassi watu hawa wakasema, Hatutaona neno juu yake Danieli huyu, tusipoona juu yake kwa mambo ya sheria ya
6 Muungu wake. Ndipo wakuu na maliwali hawa wakamjia kwa tadi mfalme wakamwambia hivi, Mfalme Dario, uishi milele. Wakuu wote wa ufalme, majemadari, na maliwali, na madiwani, na maakida wamefanya shauri pamoja kuweka sheria ya kifalme, na kutia amri imara, yee yote atakayetaka haja kwa Muungu wo wote ao kwa mwana Adamu siku thelathini, illa kwako, Ee mfalme,
8 me, atatupwa tunduni mwa simba. Haya, Ee mfalme, uiweke amri, ukatie andiko muhuri, lisibadilike, kwa sheria ya Wamedi
9 na Waajjemi, isiyopita. Bassi mfalme Dario akatia muhuri andiko na amri. Danieli alipojua ya kuwa andiko limetiwa muhuri, akaenda nyumbani ; na madirisha yake yakiwa wazi chumbani mwake kulekea Yerusalemi, akapiga magote marra tatu

DANIELI, VI.

killla siku, akaomba, akashukuru mbele
ya Muungu wake, kama alivyofanya kwa-
11 nza. Bassi watu hawa wakamjia kwa tadi,
wakamwona Danieli anataka haja, na kusi-
12 hi mbele ya Muungu wake. Wakakaribia
wakanena mbele ya mfalme kwa mambo ya
amri ya mfalme; Hukutia amri muhuri, killa
ntu atakayeomba kwa Muungu wo wote ao
mwana Adamu muda wa siku thelathini
illa kwako, Ee mfalme, atatupwa tunduni
mwa simba? Mfalme akajibu akasema, ne-
no hili la kweli, kwa sheria ya Wamedi na
13 Waajjemi isiyopita. Wakajibu wakasema
mbele ya mfalme, Danieli yule wa waana wa
mateka wa Yuda, hakuangalii, Ee mfalme,
wala ile amri uliyoitia muhuri, illa kuomba
14 anaomba marra tatu killa siku. Bassi mfa-
lme aliposikia maneno akachukiwa sana na
nafsi yake akaweka moyo wake amwokoe
Danieli: akashughulika hatta kuchwa kwa
15 jua amwokoe. Nao watu hawa wakamjia
kwa tadi mfalme, wakamwambia mfalme,
Ujue, Ee mfalme, kama sheria ya Wamedi
na Waajjemi, Isibadilike amri wala sheria

DANIELI, VI.

- 16 aifanyayo mfalme. Bassi mfalme akaamuru,
wakamleta Danieli, wakamtupa tunduni
mwa simba. Mfalme akanena akanwambi a
Danieli, Muungu wako unayemtumikia da-
17 yima ndiye atakayekuokoa. Likaletwa jiwe
likawekwa kanwani mwa tundu; mfalme
akalitia muhuri kwa muhuri yake yeye, na
kwa muhuri ya wakuu wake; kusudi lisiba-
dilike kwa Danieli.
- 18 Bassi mfalme akaenda jumbani kwake,
akafunga usiku kucha : wala vinanda haku-
19 letewa: usingizi wake ukatoka kwake.
Mfalme akaondoka assubuhi na mapema
sana, akaenda kwa haraka kwa tundu la si-
20 mba. Naye, alipofika tunduni, akamlilia
Danieli kwa sauti ya huzuni, mfalme akanē-
na akanwambia Danieli, Ee Danieli mtumwa
wa Muungu aliye hayi, Muungu wako, ū-
mtumikiaye dayima, aweza kukuokoa kati-
21 ka simba? Danieli akanwambia mfalme,
22 Ee mfalme uishi milele. Muungu wangu
amempeleka malaika wake, amefunga mā-
kanwa ya simba wasinithuru: kwa kuwa
mbele yake nimeonekana sina hatiya, wala

DANIELI, VI.

- mbele yako tena, Ee mfalme, sikukosa.
- 23 Ndipo mfalme akafurahiwa sana kwa habari zake, akaamuru wampandishe Danieli tundu-
nduni. Bassi Danieli akapandishwa tundu-
ni, wala mathara yo yote haikuonwa kwake,
kwa sababu alimwamini Muungu wake.
- 24 Mfalme akaamuru, wakawaleta wale watu waliomshtaki Danieli, wakawatupa tundu-
ni mwa simba, wao, na watoto wao, na wake
wao; simba wakawashinda, wakawavunja-
vunja mifupa yao yote, kabla hawajafika
chini ya tundu.
- 25 Bassi mfalme Dario akawaandikia watu
wote na mataifa na ndimi, wakao katika
- 26 dunia yote; Amani izidi kwenu. Nafanya
amri, katika killa mamlaka ya ufalme wa-
ngu watu watetemeke waogope mbele ya
Muungu wa Danieli: kwani yeye Muungu
aliye hayi, akaaye milele na ufalme wako
usioharibika, na mamlaka yake hatta mwi-
- 27 sho. Yeye atoaye, aokoaye, atendaye isha-
ra na mataajabu, katika mbingu na inchi,
aliyemwoko Danieli mkononi mwa simba.
- 28 Bassi Danieli huyu akafanikiwa katika ku-

DANIELI, VII.

miliki kwa Dario, na kumiliki kwa Kuro Mwajjemi.

- VII. Mwaka wa kwanza wa Belshazzar mfalme wa Babel Danieli akaona ndoto na njozi za kitwa chake kitandani mwake, bassi akaandika ndoto, akatoa jumla ya maneno.
- 2 Danieli akanena akasema, Naliona katika njozi yangu usiku, na tazama, pepo 'nne za mbinguni zikashindana juu ya bahari kuu.
- 3 Wakatoka nyama wakubwa wa'nne bahari-
4 ni walio mbalimbali. Wa kwanza kama simba, akawa na mabawa ya tai: nikawa nikitazama hatta mabawa yake yakang'olewa, akainuliwa katika inchi, akasimamishwa miguuni kama mwana Adamu, akapewa
5 moyo wa mwana Adamu. Na tazama nyama mwingine, wa pili, kama dubu, akajiinua upande mmoja, na mbavu tatu kinwani mwake kati ya meno yake: wakamwambia hivi, On-
6 doka, ukale nyama tele. Baadaye nikaona, na tazama mwingine, kama chui aliye na mabawa ma'nne ya ndege mgongoni mwake; nyama huyu tena alikuwa na vitwa vi'nne;
7 akapewa mamlaka. Baadaye nikaona ka-

DANIELI, VII.

tika njozi za usiku, na tazama nyama wa
'nne, mwenyi hofu na kuogofya, na hodari
mno; akawa na meno ya chuma makubwa:
akameza akavunjavunja, akakanyaga ma-
saliao na miguu yake; akawa mbalimbali na
nyama zote za kwanza; akawa na pembe ku-
8 mi. Nikaziangalia zile pembe, na tazama,
ikapanda kati yao pembe ngine ndogo,
mbele yake tatu za zile pembe za kwanza
zikang'olewa; na tazama, katika pembe hii
macho kama macho ya mtu, na kanwa line-
9 nalo makuu. Nikaona hatta huweka viti,
akakaa Mzee wa siku, nguo zake nyeupe
kama theluji, na nyele za kitwa chake ka-
ma suffuf iliyosafika: kiti chake ndimi za
10 moto, gurudumu zake moto uwakao. Mto
wa moto ukapita ukatoka kwa mbele yake,
elfu elfu wakamngojea, na elfu kumi marra
elfu kumi wakasimama mbele yake, huku-
11 mu ikakaa, vitabu vikafunuliwa. Ndipo
nikatazama kwa ajili ya sauti ya maneno
makuu pembe iliyoyanena: nikatazama hat-
ta nyama alipouawa, mwili wake ukaharibi-
12 ka, ukatolewa kwa moto uwakao. Wale

DANIELI, VII.

- nyama waliosalia, wakatwaliwa mamlaka yao, kwani wakapewa kuongezeka katika
- 13 maisha yao. Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, akaja, aliyefanana na mwana Adamu, na mawingu ya mbingu, akamjia
- 14 Mzee wa siku, wakamkaribisha mbele yake. Akapewa mamlaka, na utukufu, na milki, watu wote, na mataifa, na ndimi, wamtumikie, mamlaka yake mamlaka ya milele, isiyopita, na milki yake isiyocharibika.
- 15 Mimi Danieli nalihuzunika rohoni mwangu kati ya mwili, njozi za kitwa changu
- 16 zikanifathaisha. Nikamkaribia mmoja wao waliosimama karibu, nikamwuliza maana yake haya yote. Bassi akaniambia, akani-
- 17 julisha tafsiri ya mambo haya. Nyama hawa wakubwa, walio wa'nne, wafalme
- 18 wa'nne watakaoondoka katika inchi. Lakini watakatifu wake Aliye juu wataupokea ufalme, wataumiliki milele, hatta milele na
- 19 milele. Tena nikataka kujua maana yake nyama wa'nne, aliyekuwa mbali nao wote wenziwe, mwenyi hofu mno, meno yake chuma, na makucha yake shaba: akameza, na

DANIELI, VII.

kuvunjavunja na kukanyaga masalio na mi-
20 guu yake. Na ya pembe kumi za kitwani
mwake, na ile ngine iliyopanda, mbele yake
tatu zikaanguka: hatta pembe ile yenyi
macho, na kanwa lililonena makuu, na uso
21 wake hodari kuliko wenzake. Nikaona pe-
mbe ileile ikafanya vita na watakatifu,
22 ikawashinda; hatta alipokuja Mzee wa siku,
watakatifu wake aliye juu wakapewa huku-
mu, wakati ukawadia watakatifu wakami-
23 liki ufalme. Ndivyo alivyosema, nyama
wa 'nne atakuwa ufalme wa 'nne katika
inchi, utakaokuwa mbalimbali na falme
zote, na kuimeza inchi yote, na kuikanyaga,
24 na kuivunjavunja. Na pembe kumi kati-
ka ufalme huu wafalme kumi watakaopanda:
na mwingine atapanda nyuma yao; naye
atakuwa mbalimbali nao wa kwanza, naye
25 atatiisha wafalme watatu. Naye atasema
maneno juu yake Aliye juu, atawathoofisha
watakatifu wake Aliye juu, na atatumaini
kubadili wakati na sheria: nao watatolewa
mkononi mwake hatta muda na muda mbili
26 na nuss u muda. Lakini hukumu itakaa,

DANIELI, VIII.

uaye atatwaliwa mamlaka, kupoteza na ku-
27 haribu hatta mwisho. Na ufalme, na ma-
mlaka, na ukuu wa ufalme chini ya mbi-
ngu pia, watapewa watu wa watakatifu
wake Aliye juu, ufalme wake ufalme wa
milele, na milki zote watamtumikia, wata-
28 mtii. Hatta hivi mwisho wa neno. Na-
mi Danieli mawazo yangu yakanifathaisha
sana, uso wangu ukanigeukia, nikaliweka
jambo moyoni mwangu.

VIII. Mwaka wa tatu wa kumiliki kwa mfa-
lme Belshazar njozi ikanitokea mimi Danie-
2 li baada yake ile iliyonitokea kwanza. Ni-
kaona katika njozi; ikatukia, nilipoona,
nipo Shushan jumbani, katika ufalme wa
.Elam; nikaona katika njozi, nikawa kari-
3 bu na mto Ulai. Bassi nikayainua macho
yangu, nikaona, na, tazama, kuna kondoo
mume amesimama mbele ya mto, mwenyi
pembe : na zile pembe ndefu ; lakini moja
ndefu kuliko ya pili, nayo ndefu ikapanda
4 baadaye. Nikamwona kondoo mume akisu-
kuma kwa magari, na kwa kaskazini, na
kwa kusini ; wasiweze nyama wote kusima-

DANIELI, VIII.

ma mbele yake, wala kuokoa katika mkononi mwake; illa akatenda kwa nia yake, akawa mkubwa.

- 5 Nami nilipokifahamu, tazama, bebera akatoka magaribi usoni mwa dunia pia, asiguse inchi: naye bebera mwenyi pembe
6 mashuhuri kati ya macho yake. Akamjia kondoo mume mwenyi pembe niliyemwona akisimama mbele ya mto, akaenda mbio
7 juu yake na ghathabu ya nguvu zake. Nikamwona akimkaribia kondoo mume, akamwonea hasira, akampiga kondoo mume, akamvunja pembe zake mbili; wala kondoo mume hakuwa na nguvu asimame mbele yake, akamtupa chini katika inchi, akamkanyaga: wala hapana wa kumwokoa kondoo
8 mume mkononi mwake. Bassi bebera yule akakua sana: na alipokuwa hodari, pembe kubwa ikavunjika; na mahali pake zikatoka 'nne mashuhuri kwa pepo 'nne za
9 mbingu. Katika moja yao ikatoka pembe ndogo iliyokua mno, kwa kusini, na kwa
10 mashariki, na kwenyi uzuri. Ikakua juu ya jeshi la mbingu; ikaangusha chini katika

DANIELI, VIII.

- 11 jeshi na nyota, ikazikanyaga. Kutukuka
akatumuka hatta juu yake mkuu wa jeshi,
nayo ya killa siku akaondolewa, pakaangu-
12 shwa pahali pa patakatifu pake. Jeshi
likatolewa juu yake ya killa siku kwa maa-
na ya kosa, likaitupa kweli chini katika
inchi ; likatenda kazi likafanikiwa.
- 13 Ndipo nikamsikia mtakatifu mmoja kuse-
ma, na mtakatifu mwingine akasema naye
fullani aliyenena, Hatta lini njozi yake ya
killa siku, na kosa la uharibifu kutoa na
patakatifu na jeshi hatta kukanyagwa chi-
14 ni? Akaniambia, Hatta siku elfeen na mia
tatu ; ndipo patakatifu patatakasika.
- 15 Ikawa mimi, mimi Danieli, nilipoiona njo-
zi, nikaitafuta maana, ndipo, tazama, kuli-
simama mbele yangu kama mfano wa mwa-
16 na Adamu. Nikasikia sauti ya mwana A-
damu kati ya Ulai, iliyoita ikasema, Gabri-
17 eli, umjulishe huyu njozi. Bassi alikaribia
niliposimama : naye alipokuja, nikaogopa,
nikaanguka usoni pangu : naye akaniambia,
Utambue, Ee mwana Adamu : kwani hatta
18 wakati wa mwisho njozi. Bassi alipokuwa

DANIELI, VIII.

akisema nami, nalikuwa na usingizi mzito
fulifuli katika inchi: naye akanigusa akani-
19 simamisha kusimama. Naye akasema, ta-
zama, nitakujulisha nini itakayokuwa mwi-
sho wake hasira, kwani kwa muhulla iliyo-
20 amriwa mwisho. Kondoo muone uliyemwo-
na mwenyi pembe wafalme wa Umedi na
21 Ajjemi. Naye bebera mfalme wa Uyonani:
na pembe kubwa kati ya macho yake mfa-
22 lme wa kwanza. Na kwa kuvunjika ile,
zikiwa zimesimama 'nne mahali pake, fa-
lme 'nne zitasimama kutoka taifa lile, zisi-
23 we na nguvu zake. Na wakati wa mwisho
wa milki yao, watakapotimia wakosao, mfa-
lme mwenyi uso mkali, na kutambua mafu-
24 mbo, atasimama. Na uwezo wake utaku-
wa hodari, illa si kwa nguvu zake mwenye-
we: kwa ajabu ataharibu, na kufanikiwa na
kutenda, naye atawaharibu wenyi nguvu na
25 watu wa watakatifu. Na kwa mashauri
yake tena atafanikisha hila mkononi mwa-
ke; naye atatukuka moyoni mwake, na kwa
raha atawaharibu wengi: naye atasimama
juu yake mkuu wa wakuu; lakini atavunji-

DANIELI, IX.

23 ka pasipo mikono. Na njozi ya jioni na assu-
bui iliyonenwa, kweli; bassi uifunge njozi,
27 kwani ya siku nyingi. Nami Danieli nika-
zimia, nikaugua siku; baadaye nikaondoka,
nikatenda shughuli za mfalme; nikashangaa
kwa njozi, asitambue hatta mtu.

IX. Mwaka wa kwanza wa Dario mwana wa
Ahasuero, wa uzao wa Wamedi, aliyewe-
kwa mfalme juu ya milki ya Wakaldayo;
2 mwaka wa kwanza wa kumiliki kwake mi-
mi Danieli nikatambua nayo maandiko be-
sabu ya miaka, kama neno la Yahuwa lili-
vyomjia Yeremia nabii, aitimize miaka sa-
3 bwini katika ukiwa wa Yerusalemi. Nika-
mwekea Yahuwa Muungu uso wangu kuta-
ka kwa sala, na kwa kuombea, na kwa ku-
4 funga, na kwa sako, na kwa majifu. Ni-
kamwombea Yahuwa Muungu wangu, ni-
katenda kuungama kwangu, nikasema, Ee
Yahuwa, Muungu mkuu na mwenyi kuogo-
fya, ashikaye agano na rehema kwao wa-
mpendao, na kwao washikao amri zake;
5 tumekosa, tumefanya thambi, tumetenda
uovu, tumeasi, hatta kwa kuziacha amri za-

DANIELI, IX.

6 ko na hukumu zako: wala hatukuwasikiliza
watumwa wako, manabii, waliosema kwa
jina lako na wafalme wetu, na wakuu wetu,
7 na baba zetu, na watu wote wa inchi. Ee
Yahuwa kwako haki, kwetu kutahayarika
uso, kama leo hii; kwa watu wa Yuda, na
kwa wakaao Yerusalemi, na kwa Israeli
wote karibu na mbali, katika inchi zote u-
likowafukuza, kwa ajili ya kosa lao, walio-
8 kukosea. Ee Yahuwa kwetu kutahayarika
uso, kwa wafalme wetu, na kwa wakuu we-
tu, na kwa baba zetu, kwa sababu tumeku-
9 kosea. Kwa Bwana Muungu wetu rehema
10 na kusamehe, tukiwa tumemwasi; wala ha-
tukutii sauti yake Bwana Muungu wetu, tu-
ende katika sheria zake, alizoziweka mbele
11 yetu na watumwa wake manabii. Hatta
Israeli wote wamekosa katika sheria yako,
hatta kwa kuondoka, wasitii sauti yako;
kwa hiyo laana imemwagika juu yetu, na
kiapo kilichoandikwa katika torati ya Musa
mtumwa wa Muungu, kwa sababu tume-
12 mkosea. Naye ameyatimiza maneno yake
aliyoyanena juu yetu, na juu ya waamuzi we-

DANIELI, IX.

tu waliotuamua kwa kutuletea maovu ma-
kuu; kwani chini ya mbingu pia haikute-
13 ndeka, kama ilivyotendeka juu ya Yerusa-
lemi. Kama ilivyoandikwa katika torati ya
Musa, mabaya haya yote yametujia: illakini
hatukumsihi uso Yahuwa Muuugu wetu tu-
pate kugeuka katika maovu yetu, na kuta-
14 mbua kweli yako. Bassi Yahuwa ameuvizia
uovu, ametuletea: kwani Yahuwa Muungu
wetu mwenyi haki katika kazi zake zote
15 anazoitenda: kwani hatukumtii sauti. Na
sasa, Ee Yahuwa Muungu wetu, uliyewa-
leta watu wako katika inchi ya Misri na
mkono wa nguvu, ukajipatia sifa kama leo
hii; tumekosa, tumetenda vibaya.
16 Ee Yahuwa, kwa haki yako yote, naku-
sihi, hasira yako na ghathabu yako igeuke
katika mji wako Yerusalemi, mlima mtaka-
tifu wako: kwani kwa thambi zetu na kwa
maovu ya baba zetu, Yerusalemi na watu
wako wamekuwa shutumu kwa wote pande
17 zetu zote. Bassi sasa, Ee Muungu wetu,
usikie sela ya mtumwa wako na kuomba
kwake, na uso wako uangaze juu ya pata-

DANIELI, IX.

- katifu pako panapo ukiwa kwa ajili yake
- 18 Yahuwa. Ee Muungu wangu, uiname sikio lako, ukasikie, ufunue macho yako ukaone ukiwa wetu na mji, lilimoitwa jina lako, kwani si kwa haki yetu, illa kwa rehema zako zilizo kuu twakutolea kuomba kwetu
- 19 mbele yako. Ee Bwana, sikia; Ee Bwana, samehe; Ee Bwana, sikia, tenda; usikawie kwa ajili yako wewe, Ee Muungu wangu: kwani mji wako na watu wako wanakwitwa
- 20 kwa jina lako. Nami nikinena nikiomba, nikiungama thambi yangu, na thambi ya watu wangu Israeli, nikitoa kuomba kwangu mbele ya Yahuwa Muungu wangu kwa mli-
- 21 ma mtakatifu wa Muungu wangu; ndipo nikinena katika kuomba, hatta yule mtu Gabrieli, niliyemwona katika njozi mwanzo, akipelekwa kuruka upesi, akanigusa ka-
- 22 ma wakati wa sadaka ya jioni. Akanijulisha, akazumgumza nami, akasema, Ee Danieli, nimetoka sasa nikupe akili za kutambua.
- 23 Mwanzo wa kuomba kwako neno likatoka, nami nimekuja kuonyesha; kwani wewe mtu wa kutamanika: bassi utambue jambo,

DANIELI, X.

- 24 ukafahamu njozi. Juma sabwini zimekusudiwa juu ya watu wako, na juu ya mji wako mtakatifu, kukomesha makosa, na kutia muhuri thambi, na kufanya upatani-sho wa uovu, na kuleta haki ya milele, na kufunga njozi na nabii, na kumtia mafuta
- 25 Mtakatifu wa Watakatifu. Ujue bassi, ukatambue, tangu kutoka neno la kuurudisha na kuujenga Yerusalemi hatta Masiya. Mkuu, juma saba, na juma settini na mbili: mtaa utarejea utajengwa, na ukuta hatta
- 26 wakati wa shidda. Na baada ya juma settini na mbili Masiya atakatika, wala haitakuwa kwake: na watu wa jemadari atakayekuja watauharibu mji, na patakatifu; na mwisho wake kwa gharika, na hatta mwisho wa vita ukiwa umekusudiwa. Naye atakaza agano na wengi kwa juma moja: na kati ya juma atakomesha thabihu na sadaka, na kwa mabawa ya machukizo mfanya ukiwa, na hatta ukomo nao ulioamuriwa utamwagika juu yake mwenyi ukiwa.
- X. Mwaka wa tatu wa Kuro mfalme wa Ajjemi Danieli, mwenyi jina la Belteshazar

DANIELI, X.

akafunuliwa neno; nalo kweli, lakini wakati ulioamriwa mkubwa: naye akalitambua neno, akaifahamu njozi. Siku zile mimi Danieli nalikuwa nikikaa matanga juma tatu nzima. Sikula mkate wa kutamanika, wala nyama wala mvinyo haikuja kanwani mwangu, wala sikujitia mafuta kabisa, hata juma tatu nzima zilipotimia. Na siku ya aroba asharin ya mwezi wa kwanza nilipokuwako kando la mto mkubwa, ndio Hiddekel; ndipo nikayainua macho yangu, nikaona, na, tazama, mtu mmoja aliyevikwa kitani, na viuno vyake vimefungwa na thababu safi ya Ufaz: mwili wake tena kama tarshishi, na uso wake kama kuonekana umeme, na macho yake kama taa za moto, na mikono yake na miguu yake kama rangi ya shaba iliyokatuka, na sauti ya maneno yake kama sauti ya makutano. Nami Danieli peke yangu nikaiona njozi: kwani watu waliokuwa nami hawakuiona njozi: lakini tetemeko kuu likawaangukia, bassi wakakimbia wajifiche. Nami nikaachwa peke yangu, nakaiona njozi hii kuu, wala

DANIELI, X.

- lazikusalia nguvu ndani yangu: kwani uzuri wangu umebadilika mwangu kuwa
9 uharibifu, wala sikuwa na nguvu. Illa sauti ya maneno yake nikaisikia: nami niliposikia sauti ya maneno yake, ndipo nikawa na usingizi mkuu fulifuli, na uso wangu umelekea inchi.
- 10 Na tazama, mkono ukanigusa, ulioniweka katika magote na vitanga vya mikono.
- 11 Akaniambia, Ee Danieli, mtu wa kutamania, utambue maneno nikuambiayo, na kusimama usimame: kwani kwako sasa nimepelekwa. Alipolinena neno hili kwa-
- 12 ngu, nikasimama nikitetemeka. Bassi akaniambia, Usiogope, Danieli: kwani tangu siku ya kwanza ulipotia moyo wako utambue, ukajiathibu mbele ya Muungu wako, maneno yako yamesikiwa, nami nimekuja
- 13 kwa ajili ya maneno yako. Lakini mkuu wa ufalme wa Ajjemi akanizuia siku asharini na moja: na, tazama, Michaeli, mmoja wa wakuu, akaja kunisayidia; nikakaa huko
- 14 na wafalme wa Ajjemi. Sasa nimekuja nikutambulisha yatakayowapata watu wako

DANIELI, X.

- siku za mwisho : kwani njozi bado ya siku.
- 15 Naye aliponiambia maneno kama haya, nikageuza uso wangu chini, nikawa bubu.
- 16 Na, tazama, kama mfano wa waana wa Adamu akanigusa midomo yangu: ndipo nikafupua kanwa langu, nikanena, nikase-
ma naye aliyesimama mbele yangu, Ee Bwana wangu, kwa njozi huzuni zangu zi-
- 17 menigeukia, wala sina nguvu tena. Kwani awezaje mtumwa huyu wa kwana wangu kusema na huyu Bwana wangu? Kwani kwangu mimi, marra hazikusalia nguvu mwangu, wala pumzi haikukaa mwangu.
- 18 Bassi akaja tena akanigusa kama mfano wa
- 19 mwana Adamu, naye akanitia nguvu. Akasema, Ee mtu wa kutamanika, usiogope: amani kwako, uwe na nguvu, hatta, uwe na nguvu. Na aliposema nami, nikatiwa nguvu, nikasema, Bwana wangu aseme;
- 20 kwani umenitia nguvu. Bassi akasema, Wajua sababu gani nimekujia? na sasa nitarudi nipigane na mkuu wa Ajjemi: nami nitakapotoka, tazama, mkuu wa Uyo-
- 21 nani atakuja. Lakini nitakuonyesha yali-

DANIELI, XI.

yoandikwa katika maandiko ya kweli: wala hapana ajitiaye nguvu kwa mambo haya, illa Mikaeli, mkuu wenu.

- XI Tena mimi mwaka wa kwanza wa Dario Mmedi, mimi nikasimama nimthubutishe, 2 nimtie nguvu. Na sasa nitakuonyesha ya-liyo kweli. Tazama, watasimama bado wafalme watatu katika Ajjemi; naye wa 'nne atawapita wote kwa utajiri: na kwa nguvu zake atawaleta wote na utajiri wake 3 juu ya ufalme wa Uyonani. Na mfalme hodari atasimama, atakayetawala na mamlaka kuu, na kutenda kwa mapenzi yake. 4 Naye atakaposimama, ufalme wake utavunjika, utatawanyika kwa pepo 'nne za mbingu; wala si kwa watoto wake, wala kwa mamlaka yake aliyoitawala: kwani ufalme wake uta'ngolewa hatta kwao wangine wasio wale.
- 5 Na mfalme wa kusini atakuwa hodari, na wa wakuu wake; naye atakuwa hodari kuliko yeye, naye atakuwa na mamlaka; mamlaka yake mamlaka kuu. Na mwisho wa 6 miaka watasharikiana, kwani binti mfalme

DANIELI, XI.

wa kusini atamjia mfalme wa kaskasini kufanya mapatano, lakini binti hatazishika nguvu za mkono; wala mfalme hatasimama, wala mkono wake : lakini yule binti atatolewa, nao waliompeleka, naye aliyemzaa, naye
7 aliyemtia nguvu zamani zao. Lakini katika tawi la mizizi yake atasimama mahali pake, atakayekuja na jeshi, na kuingia ngome ya mfalme wa kaskazi, na kutenda
8 juu yao, na kushinda : naye atachukua tena mateka hatta Misri miungu yao pamoja na wakuu wao, na vyombo vya kutamanika vya fetha na vya thahabu; naye atakaa
9 miaka zayidi ya mfalme wa kaskazi. Bassi mfalme wa kusini atakuja kwa mamlaka,
10 atarudi inchi yake yeye. Lakini waanawe watakasirika, watakusanya wingi wa majeshi makuu : na hakika atakuja atakayegharika na kupita : ndipo yule atarudi ataamka
11 hatta ngomeni mwake. Naye mfalme wa kusini ataingiliwa na ghathabu, atatoka atapigana naye, na mfalme wa kaskazini, naye atatoa jeshi kubwa; lakini jeshi
12 litatolewa mkononi mwake. Atakapokwi-

DANIELI, XI.

sha kuchukua lile jeshi, moyo wake utainuliwa ; naye ataangusha elfu kumi, asiongezke nguvu. Kwani mfalme wa kaskazini atarudi, atatoa jeshi kubwa kuliko lile la kwanza, naye hakika atakuja mwishoni mwa wakati, ndio miaka, na jeshi kubwa na utajiri mwingi. Na nyakati zile watasimama wengi juu yake mfalme wa kusini : tena waana wenyi jeuri wa watu wako watajiinua kutimiza njozi ; lakini wataanguka. Bassi mfalme wa kaskazini atakuja, na kufanya kilima, na kuuteka mji wa maboma : wala selaha za kusini hazitashinda, wala watu wa uteule wake, wala nguvu za kushindana. Lakini yeye, ajaye juu yake, atatenda kwa mapenzi yake yeye, wala hapanana atakayesimama mbele yake : naye atasimama katika inchi ya uzuri, itakayo- haribika na mkono wake. Naye tena atakaza uso kuingia na nguvu za ufalme wake wote, na mapatano naye ; ndivyo atakavyotenda : naye atampa binti ya waana- wake, kumharibu : lakini hatasimama, wala kumsayidia. Baada yake atageuza uso wa-

DANIELI, XI.

ke kwa visiwa, atavitwaa vyingi: lakini jemadari kwake ataikomesha aibu aliyoileta; sembuse aibu yake yeye atamrudishia mwenyewe. Ndipo atageuza uso wake kwa ngome ya inchi yake mwenyewe: lakini atajikwaa ataanguka, asionekane. Bassi mmoja atasimama mahali pake apitishaye mtoza ushuru juu ya utukufu wa ufalme: lakini katika siku haba tu ataharibika, si kwa hasira, wala kwa vita. Na mahali pake atasimama mnyonge, asiyepewa nao heshima ya ufalme: lakini ataingia kwa amani, atapata ufalme kwa kujipendekeza. Na kwa mikono ya gharika watagharikiwa katika mbele yake, watavunjika; hatta naye mkuu wa agano. Na baada yake agano naye atatenda kwa hila: kwani atapanda, atakuwa hodari na watu haba. Ataingia kwa amani hatta paliponona pa ufalme; naye atatenda wasiyoyatenda baba zake, wala baba za babaze; atawatawanyia mapato na mateka na utajiri: naye ataziwazia ngome mawazo yake, hatta kwa muhulla. Naye ataamsha uwezo wake, na ushujaa

DANIELI, XI.

- wake juu yake mfalme wa kusini kwa jeshi kubwa; naye mfalme wa kusini atakasirishwa kwa vita na jeshi kubwa sana na hoda-dari, asisimame: kwani watamwazia ma-
26 wazo. Hatta walishwao na sehemu ya chakula chake wataharibu, na jeshi lake litagharikiwa: na wengi watalala wameuawa.
- 27 Na wafalme hawa wote wawili mioyo yao kufanya mathara, nao watasemana uwongo mezani pamoja; isifanikiwe: kwani bado
28 mwisho wakati ulioamriwa. Ndipo atarudi inchi yake na utajiri mwingi; na moyo wake juu yake agano takatifu; naye atate-
29 nda, na kurudi inchi yake yeye. Wakati ulioamriwa, atarudi, atakuja njia ya kusini; lakini hali yake ya kwanza, sivyo ya pili.
- 30 Kwani merikebu za Kittim zitakuja juu yake: bassi atahuzunika, atarudi, ataghatthabika juu yake agano takatifu: ndivyo atakavyotenda; kurudi atarudi, naye atawatazamia nao waliachao agano takatifu.
- 31 Na mikono itasimama upande wake, nao watatia unajisi patakatifu pa nguvu, wataiondoa ya killa siku nao wataliweka chukizo

DANIELI, XI.

- 32 la ukiwa. Nao watendao maovu juu yake
agano atawapotosha kwa maneno ya kujipe-
ndekeza: illakini watu wamjuao Muungu
33 wao watakuwa na nguvu, watatenda. Nao
wenyi hekima katika watu watafundisha
wengi: illa wataanguka na upanga, na moto,
34 na utumwa, na mateka, siku nyingi. Bassi
watakapoanguka watasayidiwa na msaada
kidogo: lakini wengi wataambatana nao
35 kwa maneno ya kujipendekeza. Na katika
wao wenyi hekima wataanguka wangine,
kuwajaribu nao, na kuwatakasa, na kuwasa-
fisha, hatta wakati wa mwisho: kwani bado
ya wakati ulioamriwa.
- 36 Na mfalme atatenda kwa mapenzi yake;
atajiinua atajivuna juu ya killa muungu,
naye atanena ya ajabu juu yake Muungu wa
miungu, naye atafanikiwa hatta ghathabu
itimizwe: kwani yaliyoyakiniwa yatafanyi-
37 ka. Wala hatamwangalia Muungu wa ba-
ba zake, wala aliyetamanika na waanawake,
wala kumwangalia muungu wo wote: kwa-
38 ni atajitukuza juu yote. Lakini mahali pa-
ke atamheshimu muungu wa ngome, na

DANIELI, XI.

muungu wasiyemjua baba zake atamheshi-
mu na thahabu na fetha na johari na yali-
39 yotamanika. Ndivyo atakavyotenda katika
ngome za maboma na muungu mgeni, ata-
kayemwungama atamwongezea utukufu :
naye atawapa kumiliki wengi, na kuwagawia
40 inchi ijara. Na wakati wa mwisho mfalme
wa kusini atamsukuma : na mfalme wa ka-
skazini atakuja juu yake kama tufanu, na
magari, na wapanda frasi, na merikebu
nyingi ; ataziingia inchi, atagharika na ku-
41 pita juu. Ataiingia inchi ya uzuri, nyingi
zitaangushwa : lakini hizi zitaokoka mko-
noni mwake, Edom, na Moab, na wa kwa-
nza wa waana wa Ammon.

42 Atatoa tena mkono wake juu ya inchi : wala
43 inchi ya Misri haitaokoka. Lakini ataku-
wa na nguvu juu ya hazina za thahabu na
za fetha, na juu ya vitu vya thamani vyote
vya Misri : nao Walibua na Wakushi nyayo-
44 ni mwake. Lakini habari zitokazo masha-
riki na kaskazini zitamtaabisha : kwa ajili
hii atatoka na ghathabu kuu, aharibu, aka-
45 waondolee wengi mbali. Naye atapanda he-

DANIELI, XII.

ma zake za kifaume kati ya bahari katika mlima mzuri wa utukufu; lakini atasalimika na ajali yake, wala hapana atakayemsayidia.

XII. Wakati ule Mikaeli atasimama, jemadari mkubwa asimamaye kwa waana wa watu wako: utakuwa na wakati wa taabu, kama usivyokuwa toka kuwa taifa hatta wakati uleule: na wakati ule watu wako wataokoka, killa atakayeonwa ameandikwa kitabuni.

2 Na wengi wao walalao katika mavumbi ya inchi wataamka, wangine kwa maisha ya milele, na wangine kwa aibu na kutharau-
3 liwa milele. Nao waalimu wata'ngaa kama mwanga wa mbingu; nao waongoao wengi kwa haki kama nyota milele na milele.
4 Lakini wewe, Ee Danieli, uyafunge maneno, ukatie muhuri kitabu, hatta wakati wa mwisho: wengi watakimbia huko na huko, na elimu itaongezeka.

5 Bassi mimi Danieli nikaona, na, tazama, wakasimama wawili tena, mmoja upande mmoja kwa mdomo wa mto, na mmoja upande
6 nde wa pili kwa mdomo wa mto. Akamwambia yule mtu aliyevikwa kitani juu ya maji

DANIELI, XII.

- ya mto, Hatta lini mwisho wa maajabu haya ?
- 7 Nikamsikia yule mtu aliyevikwa kitani juu ya maji ya mto, alipoinua mkono wake wa kuume, na mkono wake wa kushoto mbinguni, akaapa kwaye aishiye milele, kama kwa muda, na muda mbili, na nuss u muda ; naye atakapokuwa amekwisha kuzitawanya nguvu za watu watakatifu, haya yote yatati-
- 8 mia. Nikasikia, nisitambue : ndipo nikasema, Ee Bwana wangu, nini mwisho wa haya ?
- 9 Akasema, Nenda zako, Danieli : kwani kufungwa maneno na kutiwa muhuri hatta
- 10 wakati wa mwisho. Wengi watatakasika, na watasafika, na watajaribiwa ; lakini waovu watatenda maovu, wala hapana wa waovu watakaotambua ; illa wenyi hekima
- 11 watatambua. Na tangu wakati ya killa siku itakapoondolewa, na kulipandisha chukizo la ukiwa, siku elfu na miteen na tissaini.
- 12 Heri angojaye, afikaye siku elfu na mia
- 13 tatu na thelathini na tano. Lakini nenda zako wewe hatta mwisho : nawe utastarehe, na kusimama katika sehemu yako mwisho wa siku.

